**Taarifa ya Utendaji wa Baraza kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na 2021/2022**

**Mh. Naibu wa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi – Uchukuzi, Mh. Mwita Waitara,**
**Mh. Amos Makala - Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**
**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ya Temeke, Kigamboni, Ilala, Kinondoni na Ubungo,**
**Wakuu wa taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi,**
**Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini,**
**Wawakilishi wa Majukwaa ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,**
**Wawakilishi wa Vilabu vya Wanafunzi wa Sekondari na Shule za Msingi za Mkoa wa Dar Es Salaam;**
**Wageni waalikwa,**
**Sekretarieti ya Baraza,**
**Wanahabari,**
**Mabibi na mabwana.**
Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kwa kutujalia neema ya kukutana hapa kwa ajili ya uzinduzi wa tovuti ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini. (LATRA CCC). Baraza hili lipo kwa mujibu wa Kifungu Namba 29 (2) cha Sheria namba 3 ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, (LATRA) ya Mwaka 2019.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Tovuti yetu, utakayoizindua leo tarehe 01 October, 2021 imetengenezwa na Wataalamu kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na ipo kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Imezingatia mahitaji yote ya Kisheria.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Muundo wa Baraza.

Baraza lina wajumbe 07, ambapo kwa sasa wapo watano (05) wizara ipo katika hatua za kukamilisha nafasi mbili (02) za wajumbe. Baraza linaongozwa na Mwenyekiti wa Baraza. Wajumbe wa Baraza ni chombo cha juu, cha kusimamia utendaji kazi wa Baraza.

Utendaji kazi za kila siku, hufanywa na Secretariet yenye Jumla ya wafanyakazi tisa (09), kwa sasa wafanyakazi ni watano (05).

Baraza linajukumu la kuunda kamati za watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini, kwa kuwa na idadi ya wajumbe watano (05) kwa kila Mkoa. Hivi sasa, Baraza lina kamati kwenye Mikoa nane (08) ambayo ni (Kigoma, Tabora, Mtwara, Mbeya, Kagera, Tanga, Mwanza na Arusha) mikoa mingine 18 pamoja na Dar es Salaam, tupo katika hatua ya kuunda kamati hizo kwa kushirikiana na Makatibu Tawala wa Kila Mkoa, baada ya kuomba idhini kutoka kwa Katibu Mkuu TAMISEMI. Tunategemea kukamilisha uundwaji wa kamati hizi kabla ya mwisho wa Mwezi Disemba mwaka huu, 2021.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

**Dira ya Baraza**: Ni kuwa Baraza Bora kikanda katika kuwezesha na kulinda maslahi ya watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini.

**Lengo Kuu**: Ni kukuza na kulinda maslahi ya Watumiaji ili kupata uwakilishi na mwitikio mpana kwa mdhibiti, watunga será na Watoa Huduma za Usafiri Ardhini.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Kwa muda mrefu sasa, tumeshuhudia watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (Abiria) kwa njia ya Barabara, Reli na hata Majini, wakipata Huduma ambazo, wengi huishia kusema, **bora Huduma.** Kauli hii, ya kinyonge, hutokana na ukweli kuwa, abiria ambaye ndiye mlipia Huduma hupata Huduma hiyo, aidha, kwa kugombania kuingia kwenye vyombo hivyo, wakati mwingine kulazimika kulipa nauli zaidi na hivyo kukosa heshima yake ya kuwa Mteja Mfalme/Malikia. Hali hii, imesukuma Baraza kuona haja ya (Abiria) Mteja kuwa na hadhi ya Mfalme/ Malikia na Hivyo Kustahili kupata HUDUMA BORA, na SI BORA HUDUMA.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Pengine, kila mmoja wetu, anajiuliza, ni nini Baraza linaweza kufanya ili abiria aweze kuwa Mfalme katika Huduma za Usafiri Ardhini, na Hata Usafiri wa Majini? Na ni nini kifanyike ili Abiria aweze kupata HUDUMA BORA? Kwa kutambua nafasi ya Baraza katika Sekta ya Usafirishaji. Baraza lina kauli mbiu inayosema, *LATRA CCC Sauti ya Jamii.* Na tumetengeneza **Wimbo** wa Baraza, ambao pia leo tunakuomba utusaidie kuuzindua rasmi.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Baraza linatambua juhudi kubwa za Serikali, za kuboresha miundombinu, na hali nzuri ya mazingira ya uwekezaji katika Jiji la Dar Es Salaam, na Miji mingine kwenye mikoa yote Tanzania Bara. Ila kuwa na jitihada na mipango yote mizuri, Bila kuwa na

Azma ya kuwawezesha Abiria kupata Huduma ya Usafiri Kiustaarabu, bado tutakuwa na Safari ndefu ya kuwa na **Huduma Bora.**

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Baraza limeainisha mipango mikubwa mitatu, itakayosaidia abiria kupata Huduma Bora:

**Mpango wa Kwanza**: Kuhamasisha Jamii (Abiria) kuingia kwenye vyombo vya Usafiri kwa mstari. Ambao unalenga:

1. Abiria wa kwanza kufika kwenye kituo, kuwa wakwanza kupata huduma ya usafiri kiustaarabu;
2. Kuwawezesha watoto, wazee, akina mama wajawazito, wagonjwa na abiria wote kupata huduma stahiki, kwa wakati;
3. Kujenga jamii iliyostaarabika;
4. Kuponya majeraha ya muda mrefu ya abiria kuteseka vituoni
5. Kutunza vyombo vya usafiri (Milango na madirisha)
6. Kuepusha ajali na majeraha ya mwili, kupunguza uwezekano wa maambukizi ya magonjwa
7. Kuongeza, utu, umoja, upendo, mshikamano katika jamii

**Mpango WA Pili:** Kuhimiza Jamii, matumizi zaidi ya kielektroniki katika sekta ya usafirishaji; E- Tiket kwa mabasi ya Mijini na Masafa Marefu. Matumizi ya E- tiketi yatamsaidia sana abiria , kuondokana na kadhia ya Wapiga debe, kupandishiwa nauli holela, na kupata Huduma kiustaarabu.

**Mpango wa tatu:** Kukusanya maoni (Reserch) kwa jamii pana juu ya mikinzamo mbalimbali inayojitokeza katika Sekta ya Usafirishaji Nchini, na hivyo kumwathiri moja kwa moja mtumiaji wa Huduma. Mfano ajali zinazoendelea

kutokea, baadae kutumia takwimu hizo, kuishauri Sekta pamoja na Waziri mwenye dhamana na Usafirishaji,

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Baada ya kuwa na mipango, hii, tukaona ni vyema sana, Kukuomba Wewe, Mh. Mgeni Rasmi, Mh. Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi Mbalimbali za Serikali na Binafsi zilizopo hapa na nje ya hapa kupokea mipango yatu, na kuwa na mikakati endelevu ya pamoja ili kwa pamoja Abiria ambaye ndiye mwananchi aliyepo kwenye maeneo YENU aweze kupata Huduma Bora na kuwa na hadhi ya Mfalme / Malkia katika Huduma za Usafiri zilizo kiini cha maendeleo ya Uchumi wa Taifa letu.

Pamoja na Baraza kufanikiwa; kutoa elimu kwa abiria juu ya kujikinga na Maambukizi ya COVID 19 kwenye Vyombo vya Usafiri wa Umma, Kujua haki na wajibu wao, bado jitihada zaidi zinahitajika.

Ninawapongeza DART- na UDA-RT kwa kuwa mstari wa mbele kwa kuwasaidia abiria kukaa kwenye mstari, kuvaa barakoa kwenye baadhi ya vituo. Ni waombe chachu hii, iendelee kwenye vituo vingine vya BRT. Sehemu nyingine tutashirikiana na taasisi nyingine kuhamasisha ustaarabu huo.

**Mh. Mgeni Rasmi,**

Mwisho, niwaombe wageni wote, tutembelee kwenye Tovuti ya Baraza www.latraccc.go.tz itakayozinduliwa rasmi leo hii. Aidha, Baraza lina njia nyingine za mawasiliano kama: U-Tube, Tweeter, Instagram na face book. Karibuni sana.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Leo Ngowi

Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza.